

Taratibu za kufuata ili kuanzisha mashamba pori, bustani za wanyama, pamoja ranchi za wanyamapori.

1) Uanzishaji wa mashamba ya wanyamapori(wildlife farms), bustani za wanyamapori(wildlife zoo) pamoja na ranchi za wanyamapori(Wildlife ranch) unaomgozwa na kanuni zijulikanazo kama Wildlife conservation(Management of captive facility) Regulation of 2020. Kanuni ya 6 ya kanuni hiyo inaainisha sifa zifuatazo ili mtu aweze kuanzisha mashamba ya wanyamapori, bustani za wanyamapori pamoja na ranchi za wanyamapori.

- i. Muombaji anatakiwa awe na umiliki wa ardhi (hati za kumiliki ardhi). Ka ma ni forighner utaratibu wa kupewa ardhi utafuata utaratibu wa kawaida wa investment kutoka Tanzania investment center (TIC)
- ii. Awe mtanzania, kwa wageni wanatakiwa waungane na watanzania katika uwekezaji watengeneze Corporate company ambapo share iwe angalau 51% kwa watanzania na inayobaki ni kwa ngeni.
- iii. Maombi ya uanzishaji wa mashamba ya wanyamapori, bustani za wanyamapori, na ranchi za wanyamapori yaendane na mpango wa matumizi bora ya ardhi ya eneo husika.
- iv. Aandae mpango kazi (Business plan) inayoonesha uhalisia wa utekelezaji wa uwekezaji)
- v. Awe na cheti cha tathmini ya uharibifu wa mazingira (environmental impact Assessment) kulingana na aina ya wanyama anaotaka kuwafuga.
- vi. Muombaji ajiandae na utambuzi wa wanyama atakaowafuga, i.e micro-chip au alama
- vii. Alipe ada ya usajili
- viii. Muombaji awe amefuata sheria zingine zozote (zitzkazohitajika)
- ix. Afuate miongozo mingine kutoka kwa mkurugenzi wa wanyamapori.

Sambamba na usajili (registration) Muombaji atatakiwa kuwa na leseni za kujihusisha na nyara za serikali (Trophy dealer's licence) kulingana na daraja la aina ya biashara anayotaka kuifanya ambayo ni daraja la 17 ni kwa bustani za wanyamapori, 18 ni kwa mashamba ya kufugia wanyamapori na 20 ni kwa ranchi za wanyamapori

NB. Ili kuomba usajili na leseni za kujihusisha na nyara za serikali kuna maombi unatakiwa kuyatuma kwa cc@tawa.go.tz.